TANGAZO LA SERIKALI NAMBA ……LA MWAKA……..

(SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA, (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 153

SHERIA NDOGO ZA (KODI YA MAJENGO) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA, 2017

Jina na mwanzo wa kutumika	1		Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Kodi ya Majengo) ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa za mwaka 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
Matumizi	2		Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya wilaya ya Iringa.
Tafsiri	3		Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo: **"Afisa Mwidhiniwa" Maana yake ni Mweka Hazina wa Halmashauri au Afisa yeyote aliyeidhinishwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogo hizi ikiwa ni pamoja na Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji.** **"Halmashauri" Maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Iringa .** **"Kodi" Maana yake Kodi ya Majengo yote yaliyomo ndani ya Halmashauri kadiri itakavyopangwa katika jedwali.** **"Mahakama" Maana yake ni Mabaraza ya Ardhi ikiwa ni pamoja na Mahakama ya ngazi yoyote.** **"Majengo ya Biashara" Maana yake ni nyumba au sehemu yeyote ambayo inatumiwa kwa shughuli za kibiashara kama inavyoainishwa katika Jedwali.**

			"Mkurugenzi" Maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Iringa. **"Mmiliki" Maana yake ni mtu, taasisi, inayomiliki nyumba katika eneo la Halmashauri.** **"Mwangalizi" Maana yake ni mtu yeyote aliye na dhamana ya kimaamuzi juu ya nyumba iliyoko katika eneo la Halmashauri.** **"Nyumba" Maana yake ni jengo lolote lililopo ndani ya Halmashauri likihusisha maendeleo yeyote katika jengo hilo.**
Maeneo ya kutoza kodi ya Nyumba	4		Katika kutekeleza Sheria Ndogo hizi itakuwa ni wajibu wa Mmiliki au Mwangalizi wa jengo lililopo Halmashauri kulipa kodi ya jengo kwa mwaka isipokuwa:- (a) Majengo ya Serikali (b) Majengo ya Ibada (c) Makumbusho. (d) Makaburi (e) Viwanja vya michezo katika shule mbalimbali za Serikali (f) Majengo ya reli na jeshi lolote nchini.
Wajibu Mkurugenzi	5	1	Mkurugenzi atakua na wajibu wa kuhakikisha kwamba:- (a) Afisa Mwidhiniwa na maafisa walioidhinishwa wanawezeshwa kutekeleza sheria ndogo hizi. (b) Ana taarifa ya nyumba zote zilizomo katika eneo la Halmashauri. (c) Anawezesha kufanya uthamini ili kupata thamani halisi ya nyumba zilizopo katika eneo la Halmashauri kwa utaratibu utakaowekwa.
Wajibu wa Afisa Mwidhiniwa	6	1	Afisa Mwidhiniwa akishirikiana na Afisa Ardhi au Mthamini watakuwa na wajibu wa kufanya utekelezaji wa kifungu cha 5(1) ikiwa ni pamoja na: (a) Kufanya ukaguzi katika eneo lolote la Halmashauri ili kujua maendeleo ya majengo. (b) Kuandaa na kuwasilisha taarifa kwa Mkurugenzi ikijumuisha aina ya nyumba, wamiliki na maeneo

			ambayo nyumba hizo zinapatikana kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.
		2	Mtu yeyote atakayemzuia Afisa Mwidhiniwa, baada ya kujitambulisha, katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hizi au kutoa taarifa ambazo anajua si za kweli atakuwa ametenda kosa.
Eneo la Tozo	7		Halmashauri kwa kushirikiana na Waziri mwenye dhamana itatangaza eneo lote la Halmashauri kuwa eneo la tozo ya majengo kwa mujibu wa Sheria.
Wajibu wa Mmiliki wa nyumba	8	1	Utakuwa ni wajibu wa mmiliki wa nyumba: (a) kutoa ushikiano kwa Afisa Mwidhiniwa kwa kueleza ukweli juu ya umiliki na maendeleo ya nyumba husika ili kurahisisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi
			(b) Kulipa kodi ya nyumba kwa kadri itakavyoainishwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hizi.
Muda wa mwisho wa kulipa Kodi	9	1	Kila ifikapo tarehe 30 mwezi Juni ya kila mwaka itakuwa ni siku ya mwisho ya ulipaji wa Kodi.
		2	Kila Mmiliki au Mwangalizi wa nyumba atapaswa kulipa Kodi endapo atadaiwa au laa na Halmashauri kabla ya muda wa kulipa kufikia tamati kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.
Ufutaji wa Sheria Ndogo	10		Sheria Ndogo za (Kodi ya Majengo) ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa za mwaka 2001 zinafutwa.
Makosa	11	1	Itakua ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mtu yeyote: (a) Kumzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi (b) Kutoa taarifa zisizo sahihi juu ya umiliki wa nyumba
Adhabu	12		Mtu yeyote atakayeshindwa au kukataa kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi wala kupungua shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

JEDWALI LA KWANZA.

AINA YA NYUMBA	**KIWANGO CHA KODI**
1. Nyumba ya Makazi i) Kuta za Udongo na kuezekwa kwa nyasi ii)Kuta za tofali na kuezekwa kwa bati	 Tsh. 1,000/= Tsh. 2,000/=
2. Majengo ya Biashara: i) Yaliyojengwa pembezoni mwa barabara na yaliyopo katika vijiji vya: Ifunda, Tanangozi, Kalenga, Migoli, Tungamalenga, Kidamali, Itunundu, Izazi, Ismani, Ugwachanya, Mgama, Ndiwili, Nyang'oro, Idodi na Nzihi. ii) Maeneo mengine ya Halmashauri	 Tsh. 10,000/= Tsh. 5,000/=
3. Majengo ya kuishi na biashara a) Kwa mujibu wa kifungu cha 2(i) hapo juu b)Kwa mujibu wa kifungu cha 2(ii) hapo juu	 Tsh. 5,000/= Tsh. 3,000/=
4. Majengo ya Hoteli (Chakula na Malazi)	Tsh. 30,000/=
5. Migahawa i) Kwa mujibu wa kifungu cha 2 (i) hapo juu ii)Kwa mujibu wa kifungu cha 2(ii) hapo juu	 Tsh. 10,000/= Tsh. 5,000/=
6. Nyumba za kulala wageni i)Kwa mujibu wa kifungu cha 2 (i) hapo juu ii)Kwa mujibu wa kifungu cha 2(ii) hapo juu	 Tsh. 10,000/= Tsh. 5,000/=
7. Nyumba za vinywaji a) Baa i)Kwa mujibu wa kifungu cha 2 (i) hapo juu	 Tsh. 10,000/=

ii)Kwa mujibu wa kifungu cha 2 (ii) hapo juu b) Grosali i)Kwa mujibu wa kifungu cha 2 (i) hapo juu ii)Kwa mujibu wa kifungu cha 2 (ii) hapo juu c) Vilabu vya pombe za kienyeji	Tsh. 5,000/= Tsh. 5,000/= Tsh. 2,500/= Tsh. 3,000/=
8. Vituo vya Mafuta	Tsh. 20,000/=
9. Pampu za Mafuta	Tsh. 10,000/=
10. Kumbi za mikutano/burudani	Tsh. 10,000/=
11. Loji	Tsh. 30,000/=
12. Mkusanyiko wa nyumba za kuishi	Tsh. 50,000/
13. Hoteli na Mahema ya Kitalii	Tsh. 100,000/=
14. Viwanda	5% ya thamani ya majengo ya kiwanda.
15. Hospitali zinazomilikiwa na watu binafsi	Tsh. 20,000/=
16. Zahanati zinazomilikiwa na watu binafsi	Tsh. 10,000/=
17. Majengo ya shule zinazomilikiwa na watu binafsi	Tsh. 20,000/=
18. Majengo yaliyoko katika maeneo ya mashamba ya uwekezaji	Tsh. 50,000/=
19. Majengo yanayomilikiwa na taasisi za dini	Tsh. 2,000/=

Nembo ya Halmashauri ya wilaya ya Iringa imebandikwa kwenye sheria ndogo hizi kufuatia azimio la Baraza la Madiwani lililoketi mnamo tarehe…….
Na nembo hiyo imebandikwa mbele ya :-

……

ROBERT MASUNYA

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

……

STEPHEN MHAPA

MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

NAKUBALI

DODOMA

TAREHE……. **……**

GEORGE B.SIMBACHAWENE (Mb)

WAZIRI WA NCHI –OR- TAMISEMI